



American Rescue Plan

Hupunguza Gharama

ya Bima ya Afya

kwa Wakazi wengi wa

New York

**NY State of Health inaweza
kukusaidia kuelewa usaidizi
mpya wa kifedha, kusasisha
kiwango chako cha mkopo
wa ushuru na kununua na
kuchagua mpango wa afya.**

Wasiliana na NY State of Health:

 Tuma ombi mtandaoni kwenye:
nystateofhealth.ny.gov

 Piga simu Kituo cha Huduma
kwa Wateja
kwa: 1-855-355-5777
(TTY:1-800-662-1220)

 Pata usaidizi wa bila malipo
kutoka kwa Msaidizi wa
Uandikishaji. Pata kwenye:
[info.nystateofhealth.ny.gov/
findassistor](https://info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor)

*Ili kujifunza zaidi kuhusu American
Rescue Plan, tafadhali tembelea:
[https://info.nystateofhealth.ny.gov/
AmericanRescuePlan](https://info.nystateofhealth.ny.gov/AmericanRescuePlan)*

Kuelewa Usaidizi Mpya wa Kifedha

- American Rescue Plan iliidhinishwa kuwa sheria mnamo tarehe 11 Machi, 2021. Inajumuisha usaidizi mpya na mkubwa wa kifedha kwa Wakazi wa New York wanaoijiandikisha katika bima ya afya kupitia NY State of Health.
- Usaidizi huu wa kifedha unapatikana kwa **waandikishwaji wa sasa na wapya**, ikiwemo **watu walio na mapato ya juu kwa mara ya kwanza**.
- Mikopo mikubwa ya ushuru inapatikana **sasa** kwa Wakazi wa New York walio na mapato ya chini au ya wastani. Kwa mtu binafsi, haya ni mapato ya hadi \$51,040 kwa mwaka. Kwa familia, haya ni mapato ya hadi \$104,800 kwa mwaka.
- Kuanzia **Juni**, mikopo mipy ya ushuru itapatikana kwa Wakazi wa New York ambao mapato yao ni juu ya viwango hivi.
- Fuatilia ilani na barua kutoka NY State ya Health zikikuarifu kuhusu wakati mabadiliko haya yanatendeka na kile unachohitaji kufanya.

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Serikali Kuu zinazotumika na haibgui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, ulemavu, maradhi yanayohusiana na ujauzito, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

American Rescue Plan

Hupunguza Gharama ya Bima ya Afya kwa Wakazi wengi wa New York

Unachohitaji Kufanya:

Ikiwa tayari umejiandikisha katika mpango kupitia NY State of Health na unapokea usaidizi wa fedha:

- Sasa unastahiki usaidizi zaidi wa kifedha.
- NY State of Health inatuma barua mapema Aprili zikiwa na kiwango chako kipywa na kikubwa cha mkopo wa ushuru. Fuata maagizo katika barua ili kusasisha kiwango chako cha mkopo wa ushuru.
- Usiposasisha kiwango chako cha mkopo wa ushuru kufikia Juni, NY State of Health itakiongeza kwa niaba yako. Utakuwa na nafasi ya kufanya mabadiliko kwa kuingia kwenye akaunti yako ya NY State of Health, kuwasiliana na msaidizi wako wa uandikishaji, au kupiga simu 1-855-355-5777.

Ikiwa ulianza ombi la NY State of Health lakini hukujandikisha katika mpango wa afya:

- Ikiwa uliambiwa kuwa ulistahiki usaidizi wa kifedha, sasa una uwezekano wa kustahiki zaidi. Ingia tena katika akaunti yako ya NY State of Health sasa na uangalie ikiwa unastahiki mikopo mikubwa ya ushuru, kisha ununue na uchague mpango.
- Ikiwa uliambiwa awali kuwa ulistahiki usaidizi wa kifedha, sasa una uweza kuustahiki. Ingia tena katika akaunti yako ya NY State of Health Juni na uangalie ikiwa unastahiki mikopo mikubwa ya ushuru, kisha ununue na uchague mpango.

Ikiwa tayari umejiandikisha katika mpango wa NY State of Health na hupokei usaidizi wa fedha:

- Sasa unaweza kustahiki mikopo ya malipo ya ushuru.
- Mikopo hii mipya ya ushuru itapatikana kuanzia Juni. NY State of Health itakutumia barua ikibainisha kiwango chako kipywa cha mkopo wa ushuru. Maagizo kuhusu jinsi ya kutuma ombi la mkopo wako wa ushuru yatapatikana kwenye <https://info.nystateofhealth.ny.gov/AmericanRescuePlan>

Ikiwa hujajiandikisha katika mpango kupitia NY State of Health na hujawahi kuanza kutuma ombi:

- Tuma ombi sasa kwenye nystateofhealth.ny.gov ili kufahamu kile unachostahiki. Wakazi wengi wa New York wanastahiki gharama ya chini au bima ya bila malipo. Usaidizi wa kifedha ulioboreshwa unapatikana sasa ikiwa una mapato ya chini au wastani (hadi \$51,040 kwa mwaka kwa mtu binafsi, au hadi \$104,800 kwa mwaka kwa familia ya wanafamilia wanne).
- Ikiwa una mapato ya juu (zaidi ya \$51,040 kwa mwaka kwa mtu binafsi, au zaidi ya \$104,800 kwa mwaka kwa familia ya wanafamilia wanne), manufaa haya yatapatikana kupitia NY State of Health kuanzia Juni.